# Muundo wa Majina ya Mahali katika Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Majina ya Vituo vya Daladala Jijini Dar es Salaam

*Adventina Buberwa*

*Ikisiri*

Wataalamu mbalimbali (taz. Byarushengo na wenzie, 1977; Katamba, 2003; Watters, 2003; Habwe na Karanja, 2004; Matei, 2008; Kihore na *wenzie*, 2009 na Mwendamseke, 2011) waliofanya tafiti kuhusu vipengele vya kimofolojia vya nomino za Kibantu wamejikita zaidi katika nomino za kawaida ilhali nomino mahususi hususan zinazotaja mahali zikiachwa bila kushughulikiwa. Kutokushughulikiwa kwa eneo hilo labda ni kutokana na madai kuwa nomino mahususi huundwa na mizizi tu na hivyo haziwezi kuchanganuliwa kimofolojia. Madai haya yamewahi kutolewa na wanaisimu kama Agard (1984) na Habwe na Karanja (2007) kwa kutaja machache. Rugemalira (2005) tofauti na Agard (keshatajwa), na Habwe na Karanja (weshatajwa) anaeleza kuwa nomino mahususi (yakiwemo majina ya mahali) hujidhihirisha katika maumbo yake maalumu. Madai haya yanayopingana ndiyo yamechochea raghba ya kuandika makala haya yanayochunguza muundo wa majina ya mahali katika Kiswahili kwa lengo la kubainisha vijenzi mbalimbali vya majina ya vituo vya daladala jijini Dar es Salaam. Makala haya yanaongozwa na madai kwamba baadhi ya nomino zinazotaja mahali zina maumbo yake maalumu na zinaweza kuchanganuliwa kimofolojia.

## 1.0 Utangulizi

Taaluma inayoshughulikia majina ya mahali katika isimu hujulikana kama *toponimia* (Buberwa, 2010). Taaluma hii imeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali kama vile Powicke (1954), Roden (1974), Rye (2006), Msanjila na wenzie (2009), Rayburn (2010), na Buberwa (2010). Wataalamu hawa wamechunguza majina ya mahali kwa kutumia mkabala wa kiisimujamii na kubainisha mambo mbalimbali ya kiisimujamii yanayosababisha uteuzi wa majina fulani yanayorejea sehemu mahususi.

Aidha, baadhi ya watafiti wameangazia taaluma hii kwa kuzingatia mkabala wa kimofolojia. Vipengele vilivyochunguzwa hasa ni ubainishaji wa maumbo ya majina ya mahali (taz. Majapelo, 2009), kubainisha namna majina ya mahali yanavyonyambulishwa kuunda majina ya watu waishio katika eneo linalohusika (taz. Angus, 2005 na Rugemalira, 2005) na kubainisha viambishi-ngeli vinavyojitokeza katika majina ya mahali (taz. Fran, 2008; Buberwa, 2011). Kwa hakika hakuna utafiti kati ya tafiti zilizotajwa uliochunguza kuhusu muundo wa majina ya mahali ya Kiswahili, hususan majina ya vituo vya daladala. Uchunguzi pekee kuhusu majina ya mahali ya Kiswahili ni ule uliofanywa na Allen (1945) ambaye amechunguza kuhusu asili ya jina 'Dar es Salaam,' Brown (1975) ambaye ameshughulikia asili ya jina 'Bagamoyo' na Schotsman (2003) ambaye amechunguza majina ya vituo vya daladala na historia inayotokana na

majina hayo. Lengo la makala haya siyo kurudia yale yalishughulikiwa na wataalamu waliotangulia bali kuchunguza majina ya vituo hivyo kwa kuzingatia mkabala wa kimofolojia ili kubainisha muundo maalumu wa majina hayo. Data iliyochunguzwa imekusanywa kutoka katika baadhi ya barabara zinazopatikana katika jiji la Dar es Salaam. Kipengele kinachofuata kinafafanua kuhusu taaluma ya uchanganuzi wa vijenzi vya maneno.

## 2.0 Taaluma ya Uchanganuzi wa Vijenzi vya Maneno

Taaluma ya uchanganuzi wa vijenzi vya maneno imewashughulisha wataalamu mbalimbali kwa muda mrefu. Katika miaka ya 1920 hadi 1960 wanamuundo wa Kimarekani walishughulikia sana muundo wa maneno hususan katika kiwango cha mofolojia na walisisitiza kuwa sharti kila kiwango cha lugha kijitegemee. Wataalamu hawa walitambua mofimu kama kipashio kidogo cha kiuchanganuzi kinyume na wanamapokeo waliotazama neno kama kipashio kilicho kidogo zaidi (Nida, 1949). Mofimu moja au zaidi hujenga neno kamili na maneno huunganishwa kwa kutumia kanuni za lugha ili kujenga vipashio vikubwa zaidi kama vile maneno ambatani, virai, vishazi na sentensi.

Lugha mbalimbali duniani huwa na utaratibu maalumu wa kuunda maneno. Kwa mfano, katika lugha tenganishi, maneno huundwa kwa neno moja moja bila kuchanganyika na viambishi. Mifano mizuri ya lugha hizo ni kama vile Kichina na Kivietinamu. Katika lugha ambishi-bainishi kama Kiswahili, maneno huundwa kwa mfuatano bayana wa mofimu. Mofimu hizo huwa na maana moja na mizizi hudhihirika wazi bila kuchanganyika na viambishi. Kwa upande mwingine, katika lugha ambishi changamani mofimu huwa na uamilifu zaidi ya mmoja. Hivyo, mofimu moja kwa mfano, inaweza kuwakilisha njeo, nafsi kauli, na kadhalika. Aidha, katika lugha kama Kiarabu na Ciruuri mofimu huchopekwa ndani ya mzizi na huwa vigumu kutenganisha mzizi na viambishi (Mgullu, 1999 na Massamba, 2004).

Licha ya lugha ya Kiswahili kutambulika kama lugha ambishi-bainishi, majina ya mahali yamekuwa yakitazamwa kama maneno yaliyoundwa kwa mofimu moja tu na hivyo hakuna utafiti uliochunguza ruwaza za kimofolojia za majina hayo. Hivyo basi, makala haya yanaangazia vijenzi mbalimbali vya majina ya mahali ya Kiswahili hususan majina ya vituo vya daladala vinavyopatikana jijini Dar es Salaam. Sehemu inayofuata inaangazia mbinu za uundaji wa majina ya Kiswahili ya vituo vya daladala.

## 3.0 Mbinu za Uundaji wa Majina ya Vituo vya Daladala

Majina ya vituo vya daladala katika lugha ya Kiswahili hayatokei kwenye ombwe. Majina hayo hutokana na majina mbalimbali yanayotaja vitu kama miti, mimea, watu, majengo na shughuli nyingine nyingi za kijamii. Hata hivyo,

uundaji wa majina hayo huzingatia pia mbinu mbalimbali za uundaji wa maneno ya Kiswahili.

Katika Kiswahili, uundaji wa maneno hufanyika kwa kutumia mbinu za uundaji wa maneno ambazo hutawaliwa na kanuni maalumu ambazo husaidia kuzalisha maumbo ya maneno tofauti tofauti. Mbinu hizo ni kama unyambulishaji, ukopaji, ufupishaji, uhurutishaji, uhamishaji maana, mwambatano na mbinu ya kubuni (Kahigi, 2007). Mbinu ya unyambulishaji, kwa mfano, inaweza kuunda maneno yenye mofimu nyingi lakini mbinu ya mwambatano hutumia maneno kamili ambayo huunganishwa kwa mpangilio maalumu ambao ukivurugwa maana pia huvurugika (Mdee, 1986 na Wesana-Chomi, 2003). Aidha, uundaji wa majina ya vituo vya daladala unajumuisha mbinu zaidi ya hizi zilizotajwa. Mbinu zinazotumika katika uundaji wa majina hayo ni mbinu ya toponimu, mbinu ya kuhamisha maana, mbinu ya eponimu na mbinu ya mwambatano. Mbinu hizi zinafafanuliwa katika sehemu zinazofuata.

## 3.1 Mbinu ya Kuhamisha Maana

Baadhi ya majina ya vituo vya daladala huundwa kwa kutumia mbinu ya kuhamisha maana. Mbinu hii ya uhamishaji wa maana huhusisha maneno ambayo tayari yanatumika katika lugha inayohusika kwa kupewa maana mpya kabisa. Utaratibu huu wa uundaji wa maneno hufanyika kwa neno lililokuwa na uamilifu A kuchukua uamilifu B bila kubadili umbo lake (Massamba, 2004). Yafuatayo ni majina ya vituo vya daladala yanayoshadidia hoja hii:

*Jedwali 1: Mifano ya Majina ya Vituo vya Daladala Yanayotokana na Mbinu ya Kuhamisha Maana*

| *Jina la Kituo* | *Kituo Kinakopatikana* | *Kichocheo* |
|---|---|---|
| Mchicha | Barabara za Chang'ombe na Mwalimu Nyerere | Mchicha unalimwa karibu na kituo hicho |
| Usalama | Barabara ya Morogoro | Kutokana na kuwepo kwa kituo cha polisi karibu na kituo hicho cha daladala |
| Shule | Barabara za Kunduchi/Tabata/ Kiwalani | Kutokana na kuwepo kwa shule karibu na kituo husika |
| Samaki | Barabara ya Bagamoyo | Kutokana na kuwepo kwa biashara ya samaki |
| Biashara | Barabara ya Mandela | Kutokana na kuwepo kwa chuo cha biashara |

Kutokana na data iliyowasilishwa katika jedwali hili ni dhahiri kwamba uundaji wa majina ya vituo vya daladala kwa njia ya kuhamisha maana siyo wa bahati nasibu. Maneno yanayoteuliwa kuwa majina ya vituo vinavyohusika huibua fikra au dhana fulani fulani kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii kama ufafanuzi ulivyotolewa katika safu ya kichocheo. Majina ya vituo kama Mchicha na Samaki, kwa mfano, yanadokeza kuwepo kwa shughuli za kilimo cha mchicha na biashara ya samaki katika maeneo ya karibu na vituo vinavyohusika. Hivyo basi, uhamishaji wa maana unazingatia pia masuala maalumu ya kijamii ya eneo linalohusika.

### 3.2 Mbinu ya Toponimu

Hii ni mbinu ya kuunda maneno hususan majina ya mahali, kutokana na hali fulani ya kijiografia (Gichuru, 2010). Mbinu hii ni zalishi katika kuunda majina mbalimbali ya mahali. Katika Kiswahili baadhi ya majina ya vituo vya daladala yameundwa kutokana na mbinu hii ya toponimu. Chunguza mifano ifuatayo:

*Jedwali 2: Mifano ya Majina ya Vituo vya Daladala Yanayotokana na Mbinu ya Toponimu*

| **Jina la Kituo** | **Kituo Kinakopatikana** | **Kichocheo** |
|---|---|---|
| Bondeni | Barabara za Chuo Kikuu na Bagamoyo | Kuwepo kwa bonde |
| Jangwani | Barabara ya Morogoro | Eneo la wazi ambalo si zuri kwa makazi |
| Bwawani | Barabara ya Pugu | Kuwepo kwa bwawa |
| Darajani | Barabara ya Morogoro | Kuwepo kwa daraja |

Kama mifano inavyoonesha hapo juu, mbinu hii ya uundaji wa majina ya vituo vya daladala inazingatia sifa za kijiografia za maeneo yaliyo karibu na kituo kinachohusika. Hali hii inadhihirisha kuwa uundaji wa majina ya vituo vya daladala katika jamii ya Waswahili hutegemea vitu wanavyoviona katika mazingira yao na majina hayo huwa rahisi kukubaliwa na wazungumzaji wa lugha hiyo.

### 3.3 Mbinu ya Eponimu

Hii ni mbinu ya uundaji wa maneno kwa kuzingatia mtu maalumu aliyevumbua au anayehusishwa na dhana fulani katika jamii. Dhana hiyo inaweza kupewa jina kwa heshima au kama kumbukumbu ya mtu maarufu au mashuhuri. Mifano ya majina yafuatayo inashadidia hoja hii:

*Jedwali 3: Mifano ya Majina ya Vituo vya Daladala Yanayotokana na Mbinu ya Eponimu*

| Jina la Kituo | Kituo Kinakopatikana | Kichocheo |
|---|---|---|
| Kwa Nyerere | Barabara ya Bagamoyo (ya zamani) | Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| Kwa Msuguri | Barabara ya Morogoro | Mtu anayefahamika sana katika eneo hilo |
| Kwa Remmy | Barabara ya Shekilango (Sinza) | Mwanamuziki maarufu |
| Kwa Mangi | Barabara ya Morogoro | Mfanyabiashara mashuhuri |

Suala la mbinu ya eponimu kutumika katika uundaji wa majina ya mahali linashadidiwa na maelezo ya Gichuru (2010) anapoeleza kuwa mbinu ya eponimu ni maarufu katika kuunda majina ya barabara, mitaa, dawa, makampuni, taasisi na majina-chapa ya bidhaa. Hata hivyo, Gichuru (keshatajwa) hatoi ufafanuzi zaidi kuhusu namna mbinu hiyo inavyohusika katika uundaji wa majina hayo. Makala haya yamefanya uchunguzi wa awali na utafiti zaidi unahitajika ili kuchunguza suala hili muhimu.

### 3.4 Mbinu ya Mwambatano

Mwambatano ni mbinu ya kuunganisha maneno mawili au zaidi ili kuunda neno moja (Mrikaria, 2004). Katika mbinu hii maneno kadhaa ambayo tayari yako katika lugha inayohusika huunganishwa ili kuunda neno jipya. Uundaji wa majina ya vituo vya daladala katika lugha ya Kiswahili huhusisha uambatishi wa aina mbalimbali za maneno kama mifano ifuatayo inavyoonesha:

*Jedwali 4: Mifano ya Majina ya Vituo vya Daladala Yanayotokana na Mbinu ya Mwambatano*

| Jina la Kituo | Kituo Kinakopatikana | Kichocheo |
|---|---|---|
| Samaki wabichi | Barabara ya Bagamoyo | Kutokana na biashara ya samaki wabichi |
| Mnazi mmoja | Barabara ya Uhuru | Kuwepo kwa mnazi |
| Mahakama ya ndizi | Barabara ya Morogoro | Kuwepo kwa soko la ndizi |
| Magari saba | Barabara ya Morogoro | Mahali ambapo kulitokea ajali iliyosababisha magari saba kuungua |

Katika mifano hii ni dhahiri kwamba majina ya vituo hivyo yana maneno zaidi ya moja. Maneno hayo hutamkwa kwa namna inayoashiria uambatani japokuwa yalivyonukuliwa hapa yanaonekana kuachiana nafasi.

Kwa ujumla uundaji wa majina ya vituo vya daladala katika Kiswahili huzingatia mbinu mbalimbali za uundaji wa maneno. Hata hivyo, mbinu hizo hukamilishana katika uundaji wa majina ya vituo hivyo. Hii ina maana kwamba uundaji wa majina mbalimbali ya vituo vya daladala huhusisha mbinu zaidi ya moja. Mbinu zote huongozwa na uhusishaji ambao huzingatia sifa za kimaumbile, kitabia au kimatumizi au sifa zaidi ya moja. Mbinu ya eponimu kwa mfano, hujikita katika kuunda majina ya mahali kutokana na majina ya watu maarufu au mashuhuri lakini baadhi ya manenounde hujidhihirisha katika maumbo ambatani kama inavyoonekana katika Jedwali la 3. Pia, uundaji wa majina ya vituo vya daladala unaotokana na mbinu ya toponimu (taz.3.2) huhusisha pia mchakato wa unyambulishaji ambapo kiambishi mahali {-ni} hupachikwa katika mzizi ili kuunda neno jipya linalorejelea mahali kama vile *Bondeni* na *Daraja*. Hivyo basi, mbinu za uundaji wa majina ya vituo vya daladala katika lugha ya Kiswahili hutegemeana na kukamilishana ili kuunda majina yanayofuata kanuni na taratibu za lugha hiyo.

## 4.0 Muundo wa Majina ya Vituo vya Daladala katika Kiswahili

Majina ya vituo vya daladala katika lugha Kiswahili hujidhihirisha katika miundo mbalimbali. Yapo majina ambayo yameundwa kwa neno moja moja lakini mengine hujidhihirisha katika muundo wa maneno mawili au zaidi. Kwa msingi huo, majina ya vituo vya daladala yana muundo wa aina mbili yaani majina yenye muundo sahili na majina yenye muundo changamani. Sehemu ifuatayo inaangazia muundo sahili wa majina ya vituo vya daladala.

### 4.1 Muundo Sahili wa Majina ya Vituo vya Daladala

Katika Kiswahili baadhi ya majina ya vituo vya daladala hujibainisha katika muundo wa neno moja tu. Muundo wa majina ya aina hii unaweza kuwa na muundo wa mzizi na kiambishi mahali (MZ+KM), kiambishi awali na mzizi (KA+MZ), au kiambishi awali, mzizi na kiambishi mahali (KA+MZ+KM). Miundo hii inaelezwa kwa kina katika sehemu zinazofuata.

#### 4.1.1 Muundo wa KA + MZ

Majina ya vituo vya daladala yenye muundo huu wa KA + MZ hutokana na shughuli mbalimbali za kibiashara (majina kama: Biashara, Samaki); shughuli za kijamii (taz. majina kama: Usalama, Shule) na miundombinu mbalimbali (kama Tengo, Reli). Tazama mifano ifuatayo:

*Jedwali 5: Mifano ya Majina ya Vituo vya Daladala yenye Muundo wa KA+MZ*

| **Jina la Kituo** | **Kiambishi-ngeli** | **Mzizi** | **Kituo Kinakopatikana** |
|---|---|---|---|
| Usalama | u- | salama | Barabara ya Morogoro |
| Makuti | ma- | kuti | Barabara ya Mlandizi |
| Mchicha | m- | chicha | Barabara ya Chang'ombe |
| Shule | N- (ngeli- N/N) | shule | Barabara za Kunduchi/Tabata/ Kiwalani |

Majina yaliyotajwa katika jedwali la 5 huundwa kutokana na nomino za kawaida ambazo hurejelea vitu maalumu vinavyopatikana katika eneo linalohusika. Aidha, maumbo ya majina hayo huchukuliwa kama yalivyo bila badiliko lolote la kiumbo. Uundaji huu wa maneno umeelezwa katika kipengele cha (3.1) cha makala haya kwamba majina ya aina hii hutokana na mbinu ya uhamishaji wa maana. Viambishi awali katika majina haya vinaweza kuwa katika umoja ama wingi kutegemeana na idadi ya vitu ambavyo kwavyo majina hayo ya vituo yameundwa. Kwa mfano, jina kama vile *makuti* lipo katika wingi ambapo katika umoja ni *kuti*.

### 4.1.2 Muundo wa MZ + KM

Majina ya vituo vya daladala yaliyo katika muundo huu wa MZ + KM hutokana na majina mbalimbali yanayotaja maumbile ya kijiografia. Chunguza mifano ifuatayo:

*Jedwali 6: Mifano ya Majina ya Vituo vya Daladala yenye Muundo wa MZ + KM –ni*

| **Jina la Kituo** | **Mzizi** | **Kiambishi Mahali {-ni}** | **Kituo Kinakopatikana** |
|---|---|---|---|
| Relini | reli | {-ni} | Barabara ya Pugu |
| Darajani | daraja | {-ni} | Barabara ya Morogoro |
| Bondeni | bonde | {-ni} | Barabara za Bagamoyo na Chuo Kikuu |
| Bwawani | bwawa | {-ni} | Barabara ya Pugu |
| Jangwani | jangwa | {-ni} | Barabara ya Morogoro |

Mifano iliyotajwa hapo juu inadhihirisha kuwa majina ya vituo vya daladala hutokana na nomino za kawaida ambazo hurejelea vitu vinavyopatikana katika maeneo yanayohusika. Aidha, kiambishi mahali {-ni} hupachikwa katika mzizi ili kuunda majina ya mahali fulani fulani. Majina ya vituo vya daladala katika kategoria hii yakitazamwa kwa msingi wa kimofolojia yametokana na mchakato wa unyambulishaji. Hata hivyo, uteuzi wa mizizi inayohusika katika uundaji wa majina haya umezingatia hali au maumbile ya kijiografia ya maeneo yanayohusika. Kama ilivyoelezwa, (taz. 3.4) mbinu za unyambulishaji na toponimu zimetumika katika kuunda majina ya vituo vya daladala vinavyopatikana katika kategoria hii. Hali hii inaibua hoja nyingine kwamba huenda uundaji wa maneno mengine tofauti na majina ya mahali katika lugha ya Kiswahili huhusisha mbinu zaidi ya moja. Suala hili linahitaji uchunguzi zaidi ili kubaini kama hali hii hujitokeza katika uundaji wa majina ya mahali tu ama hata katika uundaji wa aina nyingine za maneno.

### 4.1.3 Muundo wa KA + MZ + KM

Baadhi ya majina ya vituo vya daladala yanajidhihirisha katika muundo wa kiambishi awali, mzizi na kiambishi mahali {-ni}. Mifano ifuatayo inashadidia hoja hii:

*Jedwali 7: Mifano ya Majina ya Vituo vya Daladala yenye Muundo wa KA +MZ + KM*

| Jina la Kituo | Kiambishi awali (ngeli) | Mzizi | Kiambishi Mahali -ni | Kituo Kinakopatikana |
|---|---|---|---|---|
| Mwembeni | mw- | embe | -ni | Barabara ya Pugu |
| Mbuyuni | m- | buyu | -ni | Barabara za Bagamoyo/ Tabata/Ali Hassan Mwinyi |
| Kijiweni | ki- | jiwe | -ni | Barabara ya Shekilango |
| Msikitini | m- | sikiti | -ni | Barabara za Pugu/ Mburahati/ Kimweri |
| Magengeni | ma- | genge | -ni | Barabara ya Yombo vituka |

Majina yaliyotajwa katika Jedwali la 7 yametokana na majina mbalimbali ya vitu kama miti na majengo ambavyo vinapatikana mahali ambapo vituo hivyo hupatikana. Viambishi awali katika majina hayo ni viambishi-ngeli vya umoja ama vya wingi ambavyo vinaukiliwa na nomino za kawaida ambazo kwazo majina ya vituo hivyo vya daladala yameundwa. Aidha, kiambishi mahali {-ni}

kimepachikwa katika mzizi ili kuunda maneno mapya yanayorejelea vituo vya daladala vinavyohusika.

### 4.2 Muundo Changamani wa Majina ya Vituo vya Daladala

Majina ya vituo vya daladala katika kundi hili huundwa na maneno mawili au zaidi. Maneno ya Kategoria moja au tofauti huambatanishwa ili kuunda neno moja, kama tulivyodokeza katika sehemu 3.4 ya makala haya. Maneno yanayoambatanishwa hufuata mpangilio maalumu ambao ukivurugwa maana pia huvurugika. Majina ya vituo vya daladala katika kundi hili hujidhihirisha katika miundo maalumu ifuatayo:

#### 4.2.1 Muundo wa Nomino na Kivumishi

Baadhi ya majina ya vituo vya daladala katika lugha ya Kiswahili hujibainisha katika muundo wa nomino na kivumishi kama mifano ifuatayo inavyoonesha:

*Jedwali 8: Mifano na Majina ya Vituo vya Daladala yenye Muundo wa Nomino na Kivumishi*

| Jina la Kituo | Nomino | Kivumishi | Kituo Kinakopatikana |
|---|---|---|---|
| Samaki wabichi | samaki | wabichi | Barabara ya Bagamoyo |
| Mnazi mmoja | mnazi | mmoja | Barabara ya Uhuru |
| Magari saba | magari | saba | Barabara ya Morogoro |
| Namba tano | namba | tano | Barabara ya Mandela |
| Namba tatu | namba | tatu | Barabara ya Mandela |

Majina ya vituo vya daladala katika kategoria hii yameundwa na neno kuu ambalo ni nomino na maneno mengine yanayotoa taarifa zaidi kuhusu neno hilo kuu. Uhusiano uliopo baina ya maneno yanayounda jina moja hujulikana kama uhusiano wa maneno ambatani kiinindani (taz. Bauer, 1983 na Katamba, 1993). Hii ina maana kwamba jina moja limeundwa na maneno zaidi ya moja ambapo neno mojawapo ndilo lililobeba maanamsingi (nomino) na maneno mengine yanatoa maelezo kuhusu neno hilo (kivumishi).

#### 4.2.2 Muundo wa Kihusishi na Nomino

Majina ya vituo vya daladala katika muundo wa kihusishi na nomino yameundwa na kihusishi na jina la mtu maalumu. Uteuzi wa jina la mtu ambalo hutumika katika kuunda majina ya vituo vya daladala hutegemea umaarufu wa

mtu au mtu ambaye ni (alikuwa) mashuhuri au alikuwa wa kwanza kuishi katika eneo linalohusika. Mifano iliyofafanuliwa hapa chini inaonesha kuwa si kila jina la mtu hutumika katika kuunda majina ya vituo vya daladala. Chunguza mifano ifuatayo:

*Jedwali 9: Mifano ya Majina ya Vituo vya Daladala yenye Muundo wa Kihusishi na Nomino*

| Jina la Kituo | Kihusishi | Jina la mtu | Ufafanuzi | Kituo Kinakopatikana |
|---|---|---|---|---|
| Kwa Remmy | kwa | Remmy | Mwanamuziki mashuhuri | Barabara ya Shekilango |
| Kwa Mangi | kwa | Mangi | Mfanyabiashara maarufu | Barabara ya Morogoro |
| Kwa Nyerere | kwa | Nyerere | Rais wa kwanza, Tanzania | Barabara ya Bagamoyo |
| Kwa Msuguri | kwa | Msuguri | Mtu anayefahamika sana katika eneo hilo | Barabara ya Morogoro |

Mifano iliyoorodheshwa katika jedwali la 9 inaonesha kwamba majina ya vituo vya daladala yenye muundo wa kihusishi na nomino hufuata taratibu za uundaji wa virai vihusishi katika lugha ya Kiswahili ambapo kihusishi hutangulia na nomino hufuata kama kijalizo cha kihusishi hicho. Hivyo basi, uundaji wa majina ya vituo vya daladala katika lugha ya Kiswahili unazingatia kanuni na taratibu za lugha hiyo.

### 4.2.3 Muundo wa Nomino, Kihusishi na Nomino

Pia, majina ya vituo vya daladala katika Kiswahili hujibainisha katika muundo wa nomino, kihusishi na nomino. Mifano ifuatayo inafafanua hoja hii:

*Jedwali 10: Mifano ya Majina ya Vituo vya Daladala yenye Muundo wa Nomino, Kihusishi na Nomino*

| Jina la Kituo | Nomino | Kihusishi | Nomino | Kituo Kinakopatikana |
|---|---|---|---|---|
| Mahakama ya Ndizi | mahakama | ya | ndizi | Barabara ya Morogoro |
| Mtaa wa shoka | mtaa | wa | shoka | Barabara ya |
| Chama cha mapinduzi | chama | cha | mapinduzi | Barabara za Kunduchi/Kimweri/Morogoro |

Muundo wa majina ya vituo vya daladala katika kategoria hii umefuata kanuni na taratibu za uundaji wa virai nomino katika lugha ya Kiswahili. Nomino ya kwanza ni neno kuu wakati maneno mengine yanaelezea zaidi kuhusu neno kuu.

Aidha, uundaji wa majina yaliyotajwa katika mfano wa (10) hapo juu yametokana na mbinu ya uundaji wa maneno ya mwambatano ambapo maneno zaidi ya moja yameambatanishwa ili kuunda jina moja la kituo cha daladala. Hata hivyo mbinu ya kuhamisha maana imetumika pia kwani maneno ambayo tayari yalikuwa yakitumika katika Kiswahili yamepewa uamilifu mpya wa kurejelea mahali. Majina kama Chama cha Mapinduzi na Mahakama ya ndizi kwa mfano, ni majina ambayo yalikuwa yakitumika ambapo jina Chama cha Mapinduzi ni jina la chama cha siasa na Mahakama ya ndizi ni jina la soko. Hivyo, majina ya daladala hayatokei kwenye ombwe bali yanatokana na masuala mbalimbali ya kijamii ambamo majina hayo yanatumika.

## 5.0 Suala la Jina Moja Kurejelea Vituo vya Daladala zaidi ya Kimoja

Katika data iliyokusanywa na kuchunguzwa kwa ajili ya makala haya imebainika kwamba baadhi ya majina ya vituo vya daladala yanarejelea vituo zaidi ya kimoja ambavyo vinapatikana katika barabara tofauti. Tazama mifano ifuatayo:

*Jedwali 11: Mifano ya Majina ya Vituo vya Daladala Yanayorejelea Vituo zaidi Kimoja*

| Jina la Kituo | Mahali Kinakopatikana |
|---|---|
| Chama cha Mapinduzi | (i) Barabara ya Kunduchi<br>(ii) Barabara ya Kimweri<br>(iii) Barabara ya Morogoro |
| Shule | (i) Barabara ya Kunduchi<br>(ii) Barabara ya Tabata<br>(iii) Barara ya Kiwalani<br>(iv) Barabara ya kinondoni |
| Bondeni | (v) Barabara ya chuo Kikuu<br>(vi) Barabara ya Bagamoyo |
| Mchicha | (vii) Barabara ya Nyerere<br>(viii) Barabara ya Chang'ombe |

Mifano iliyotajwa hapo inadhihirisha kuwepo kwa majina ya vituo vya daladala yanayorejelea vituo zaidi ya kimoja. Kwa kuwa lengo la makala haya lilikuwa ni kuchunguza muundo wa majina hayo, sababu zinazoelezea kuwepo kwa hali hiyo hazikushughulikiwa.

## 6.0 Hitimisho

Ingawa kuna wataalamu mbalimbali wanaodai kwamba nomino mahususi yakiwemo majina ya mahali huundwa kwa mizizi tu na hivyo haziwezi kuchanganuliwa kimofolojia, makala haya yanabainisha kwamba majina ya

mahali ya Kiswahili hususan yanayorejelea vituo vya daladala yanajibainisha katika maumbo mbalimbali yanayoweza kuchunguzwa kimofolojia. Kwa hiyo, madai ya kwamba nomino za pekee huundwa na mizizi tu yanahitaji kutazamwa kwa jicho la kiutafiti zaidi ili kuepuka maelezo yasiyokuwa na mashiko. Makala haya yamebainisha kuwa maumbo ya majina ya Kiswahili ya vituo vya daladala yanaweza kujibainisha katika muundo wa neno moja moja au muundo wa maneno mawili au zaidi. Baadhi ya Majina hayo yanarejelea vituo zaidi ya kimoja suala ambalo limeonekana kuhitaji kuchuzwa kwa kina zaidi ili kubaini sababu zinazoelezea hali hiyo. Zaidi ya hayo, makala yamebainisha mbinu mbalimbali za uundaji wa majina ya Kiswahili ya vituo vya daladala. Mbinu hizo ni kama vile mbinu ya kuhamisha maana, mbinu ya toponimu, mbinu ya mwambatano na mbinu ya eponimu. Ni muhimu pia kusema kwamba majina hayo huundwa kutokana na mbinu za uundaji wa maneno zaidi ya moja kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 4.1.2. Kwa hakika eneo la toponimia ni pana na ni changamani kiasi kwamba makala kama haya yasingeweza kutosha kueleza masuala yote yanayohusu majina ya mahali ya Kiswahili. Hivyo basi, tafiti zaidi zinahitajika katika eneo hili la toponimia.

## Marejeo

Agard, F.B. (1984). *A Course in Romance Linguistics: A Synchronic View.* USA: Georgetown University Press.

Allen, J.W.T. (1945). "The Name Dar es Salaam." Katika *Tanganyika Notes and Records* (hence TNR). Na. 19, Kur. 67 – 68.

Angus, R. D. (2005). "Place Name Morphology and the People of Los Angeles." Katika *California Linguistics Notes*. Juz. 30. Na. 2. Kur. 1 – 8.

Bauer, L. (1983). *English Word Formation.* Cambridge: Cambridge University Press.

Brown, W.T. (1973). "East African Place Names: An Etymological Inquiry." Katika *Africana Marburgesia.* Juz. 6. Na: 1. Kur. 3 – 16.

Buberwa, A. (2011). "Viambishi-ngeli katika Nomino za Pekee: Mifano Kutoka katika Majina ya Mahali ya Kihaya." *Kiswahili,* Juz. *74.* Kur. 41 – 48.

Buberwa, A. (2010). "Investigating Sociolinguistic Aspects of Place Names in Ruhaya in North-Western Tanzania." Unpublished M.A. Dissertation, University of Dar es Salaam.

Buberwa, A. (2010). Upekee wa Nomino Mahususi: Uchunguzi Kifani wa Majina ya Mahali ya Kihaya." Katika *Kioo cha Lugha,* Juzuu, 8. Kur. 9-15.

Byarushengo, E; A. Duranti na L. Hyman. (1977). *Haya Grammatical Structure.* Los Angeles: University of Southern California.

Fran, C. (2008). "Names, Derivational Morphology and Old English." Katika *Studia Anglica Posnaniensia: International Review of English Studies.* http:/www.thefreelibrary.com/Names+derivational+morphology+and+old+English+gender, imepakuliwa tarehe 5/2/2012.

Gichuru, T.M. (2010). "Uchanganuzi wa Nomino Ambatani za Kiswahili: Mtazamo wa Mofolojia Leksia." Tasnifu ya Umahiri, Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Habwe, J na P. Karanja. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix.

Kahigi, K. (2007). "Ujanibishaji wa Office 2003 na Windows XP kwa Kiswahili Sanifu." Katika *Kioo cha Lugha, Jarida la Kiswahili na Fasihi.* Juzuu la 5. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Katamba, F. (2003). "Bantu Nominal Morphology." Katika Nurse, D. na G. Philipson (ed). *The Bantu Languages.* London na New York: Routledge. kur. 103 – 120.

Katamba, F.(1993). *Morphology.* London: The Macmillan Press Ltd.

Kihore, Y. M, Massamba, D. P.B na J. I Hokororo. (2008). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI

Majapelo, M.L. (2009). "Morphology and Semantics of Proper Names in Northern Sotho." Katika *South African Journal of African Languages*. Juz. 2. Kur. 185 – 194.

Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Matei, A. (2008). *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Mdee, J.S. (1986). *Kiswahili Muundo na Matumizi yake*. Nairobi: International Publishers.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mrikaria, G. (2004). *Kategoria za Kisarufi katika Uundaji wa Maneno*: Mradi wa Kuswahilisha Programu Huria. Warsha ya Arusha, Novemba 1-5. Arusha, Tanzania.

Msanjila, Y. P, Y. M Kihore na D. P. B. Massamba, (2009). *Isimujamii: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Mwendamseke, F.(2011). "Uainishaji wa Ngeli katika Lugha ya Kibena.Tasnifu ya Umahiri, Haijachapishwa." Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nida, E.A. (1949). Morphology: *A Descriptive Analysisi of Words. Michigan*: Michigan University Press.

Rayburn, A. (2010). *Place Names-The Canadian Encyclopedia-Historical-Dominion Reed, A.W. (1975) Place names of New Zealand*, Wellington: A.H. & A.W. Reed.

Roden, D. (1974). "Some Geographical Implications from the Study of Ugandan Place-names." In East *African Geographical Review*. Juz 12, kur. 77- 86.

Rugemalira, J.M. (2005). *A Grammar of Runyambo*. Dar es Salaam: Language of Tanzania Project, University of Dar es Salaam.

Rye, J. (2006). *A Popular Guide to Norfolk Place-names*. Guist Bottom: Larks Press.

Schotsman, P. (2003). "Place-names and History in Dar es Salaam, Tanzania." Netherlands: Leiden University.

Watters, J.R. (2003). "Grassfields Bantu." Katika Nurse, D. na G. Philippson (wahariri). *The Bantu Languages*. London: Routledge.

Wesana-Chomi, E. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili*. Sebha Libya: Chuo Kikuu cha Sebha.